

KANUNI ZA MPANGO WA WIC

Kanuni za Mpango wa WIC zitakusaidia kuelewa jinsi WIC inavyofanya kazi. Tafadhali fuata Kanuni. Kushindwa kufuata kanuni hizi kunaweza kusababisha kuondolewa kwenye WIC hadi miezi 12. Pia, unaweza kulazimishwa kulipa WIC, kwa pesa taslimu, thamani ya hundi za cheki za WIC ulizotumia. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu kanuni hizi, ***tafadhali*** wasiliana na ofisi ya WIC. Wahudumu watafurahi kukusaidia.

Unachopaswa kufanya

- Toa maelezo sahihi na ya kweli.
- Wasilisha hundi za cheki za WIC katika tarehe zilizochapoishwa kwenye cheki.
- Wasilisha hundi za cheki cha WIC kwa vyakula vilivyoidhinishwa vya WIC pekee.
- Wasilisha na utie saina hundi za cheki za WIC kwenye maduka ya mboga pekee.
- Ripoti hundi za cheki za WIC zilizopotea au kuibiwa kwa ofisi ya WIC mara moja.
- Zingatia miadi yako ya WIC au piga simu kwa ofisi ya WIC ili kupanga upya.
- Walete watoto wako na rekodi zao za chanjo kwa kila miadi ya uthibitishaji.
- Beba kitambulisho chako (ID), thibitiisho la anwani yako, na thibitisho la mapato kamili kwa kaya yako kwa kila miadi ya uthibitishaji.
- Arifu WIC kuhusu mabadiliko yoyote katika makubaliano ya ulezi ya mtoto wako au makazi mara moja.
- Chagua mtu (mbadala) wa kuchukua na kuwasilisha hundi zako za cheki za WIC kwa ajili yako au kama huwezi kufika kwenye ofisi ya WIC au duka la mboga. Mtu wako mbadala atalizika kufunzwa na wahudumu wa WIC kuhus jinsi ya kutumia hundi hizo za cheki za WIC.
- Watendee wahudumu wa WIC na mboga kwa heshima.
- Bakia na risiti za mauzo za ununuzi wa kibinafsi (zilionunuliwa kwa pesa zako mwenyewe) za vyakula vya WIC au fomula iwapo ungependa kuuza au kuzibadilisha.

Usichopaswa kufanya

- Usipeane hundi za cheki, chakula, au fomyula za WIC.
- Usiuze au kubadilisha, ikiwa ni pamoja na mtandaoni, hundi za cheki za WIC, chakula au fomyula ili upate pesa, mkopo, au vitu vingine.
- Usiwasilishe hundi za cheki za WIC ulizoripoti zimepotea au kuibiwa.
- Usiwasilishe hundi za cheki za WIC za watoto ambao hawaishi na wewe tena.
- Usibadilishe kitu chochote kwenye hundi za cheki za WIC au Kadi yako ya ID.
- Usimruhusu mtu yeyote isipokuwa mtu wako mbadala aliyeidhinishwa wa WIC kutumia hundi za cheki za WIC na Kadi ya ID. Ikiwa mtu wako mbadala atafanya kitu chochote kibaya na hundi zako za cheki za WIC, unaweza kuondolewa ili usishiriki katika WIC
- Usishiriki katika WIC katika zaidi ya kituo kimoja cha WIC katika kipindi kimoja, aidha katika Pennsylvania au katika jimbo lingine.
- Usijaribu kununua vyakula vyovyote ambavyo haviko kwenye orodha ya sasa wa vyakula vya WIC.
- Usiuze, kuazima au kubadilisha pampu ya maziwa ya mama ambayo umepokea kutoka kwa Mpango wa WIC.

Kulingana na kanuni na sera za haki za raia za sheria ya haki za kiraia na Idara ya Marekani ya Kilimo (USDA), USDA, Mashirika yake, ofisi, na wafanyakazi, na taasisi zinazoshiriki katika mipango ya kutoa USDA zimekatanzwa dhidi ya kubagua kulingana na umbari, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, ulemavu, umri, au kuadhibiwa au ulipizaji kisasi kwa shughuli za haki za kiraia katika mpango au shughuli yoyote iliyotekelezwa au kufadhiliwa na USDA.

Watu walemavu ambao wanahitaji njia nyingine za mawasiliano ya maelezo ya mpango (k.m. Braili, chapa kubwa, kanda ua sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani, n.k.), wanapaswa kuwasiliana na Shirika (Jimbo au la ndani) ambalo waliomba faida. Watu ambao hawasikii, wana ugumu wa kusikia au wana matatizo ya kuongea wanaweza kuwasiliana na USDA kupitia Huduma ya Federal Relay Service, nambari ya simu (800) 877-8339. Licha ya hayo, maelezo ya mpango yanaweza kupatikana katika kugha nyingine kando na Kiingereza.

Ili kuwasilisha malalamiko ya mpango kuhusu ubaguzi, kamilisha [Fomu ya Malalamiko ya Ubaguzi dhidi ya Mpango wa USDA](#), (AD-3027) inayopatikana mtandaoni kwenye: http://www.ascr.usda.gov/complaint_filing_cust.html, na katika ofisi yoyote ya USDA, au andika barua kwa USDA na uandike kwenye barua maelezo yote yaliyoombwa katika fomu. Ili kuomba nakala ya fomu ya malalamiko, piga simu kwa (866) 632-9992. Wasilisha fomu au barua yako iliyokamilishwa kwa USDA kupitia@

- (1) Barua: U.S. Department of Agriculture
Office of the Assistant Secretary for Civil Rights
1400 Independence Avenue, SW
Washington, D.C. 20250-9410;
- (2) Faksi: (202) 690-7442; au
- (3) Barua pepe: program.intake@usda.gov.

Taasisi hii inatoa nafasi sawa.

Swahili-WIC Program Rules